# TOFAUTI ZA MSINGI KATI YA TUNGO NOMINO NA TUNGO VITENZI KATIKA KISWAHILI

Y.P. Msanjila

## 1.0 UTANGULIZI

Uchambuzi wa tungo nomino za Kiswahili umewahi kufanywa na wanaisimu kadhaa kama Ashton (1944); Maw (1969); Yahya-Othman (1976) na Closs-Kondo Mbaye (1967). Uchambuzi wa Ashton umehitimisha kwamba tungo nomino za Kiswahili zaweza kugawanywa katika sehemu mbili:

(i) tungo nomino zenye kitenzi -KUWA;

(ii) tungo nomino zisizo na -KUWA, bali zina kopula[1] "ni" n.k.

Kimsingi -KUWA ni kipashio kimojawapo cha kopula katika tungo nomino. Ili kutofautisha kiumbo, tungo nomino zisizo na -KUWA hujengwa na "vitenzi-ungio"[2] kama vile "ni" n.k. Jambo la msingi hapa ni kwamba kitenzi -KUWA na vitenzi -ungio, vyote ni kopula, vinafanya kazi ya kutambulisha tungo nomino za Kiswahili. Makala haya yamekusudia kuchunguza:

(i) sifa za msingi za tungo nomino; na

(ii) tofauti kati ya tungo nomino na tungo vitenzi

## 2.0 MAANA YA TUNGO NOMINO NA TUNGO VITENZI

### 2.1 Tungo Nomino ni nini?

Fasiri ya tungo nomino imetokana na lugha ya Kiingereza "nominal sentences" au "non-verbal sentences". Kwa mujibu wa makala haya, 'tungo nomino' inaelezwa kuwa ni: "Kifungu cha maneno chenye maana kinachotumia kitenzi-ungio na kitenzi-KUWA kama kiarifu". Hebu tuangalie mifano michache ya tungo nomino zifuatazo:

(i) Watoto wa shule ni wakulima stadi

(ii) Mwalimu alikuwa shuleni

(iii) Daktari wa meno yuko Dodoma.

Katika sentensi (i-iii) za hapo juu, "ni", -"kuwa" na "yuko" zote ni kopula. Katika kuziainisha, ni na yuko ni mifano ya vitenzi-ungio na alikuwa ni kitenzi -kuwa.

Kwa ufafanuzi zaidi ni kwamba tungo nomino hazitumii vitenzi kamili[3] katika tungo zake. Tungo nomino hujipambanua kutoka tungo vitenzi kwa kuwepo kopula ambayo huwa ni kiungio kati ya $KN_1$ (kifungu Nomino cha kwanza) na $KN_2$ (Kifungu Nomino cha pili).

## 2.2 Tungo vitenzi ni nini?

Tungo kitenzi ni "kifungu chochote cha maneno kuanzia neno moja na kuendelea chenye kitenzi kamili na kinachotoa maana". Tungo vitenzi ni zile sentensi zenye vitenzi kamili ndani yake. Mifano ya tungo vitenzi ni kama ifuatavyo:

(iv) Anakula

(v) Musa anasoma kitabu

(vi) Ali alikuwa akicheza mpira kwa nguvu.

Kutokana na mifano hiyo hapo juu, -kula, -soma na -cheza ni vitenzi kamili. Mfano wa sentensi ya (vi) alikuwa si kitenzi kamili, bali ni kisaidizi cha kitenzi -cheza.

## 3.0 SIFA ZA MSINGI ZA TUNGO NOMINO ZA KISWAHILI

## 3.1 Kiungio Nomino cha ni/si

Sifa mojawapo ya tungo nomino za Kiswahili ni kwamba zina kiungio Nomino cha ni. Katika ukanusho kiungio si hutumika. Viungio hivi huunga $KN_1$ na $KN_2$

(vii) Baba ni mganga

(viii) Baba si mganga

Katika mazingira fulani, $KN_1$ na kiungio Nomino ni zaweza kudondoshwa zisitumike na bado tungo hiyo ikaleta maana. Kwa mfano, kama $KN_1$ kinafahamika na wazungumzaji, basi $KN_1$ huweza kudondoshwa.

(ix) Juma ni daktari? (Swali)

(x) (ndiyo) ni daktari

(xi) Ø si daktari

Wakati mwingine kiungio Nomino ni chaweza kudondoshwa ikiwa tungo hiyo itasemwa kwa kuzingatia kiimbo fulani.

(xii) Juma daktari

Katika kutamka Juma, mzungumzaji itambidi apumzike kidogo ndipo atamke daktari, kwa kiimbo cha kushusha. Hata hivyo, mfano huu wa (xii) hauonyeshi wazi kama maana inayotakiwa ni ya kukanusha. Kwa hali hiyo, ni vigumu kuacha alama ya kanusho si katika tungo yenye maana ya kanusho.

Kimsingi ni kwamba $KN_1$ na kopula ni/si vyaweza kudondoshwa katika mazingira fulani, $KN_2$ ni cha muhimu kuwepo. Muundo wa tungo za namna hii huweza kuelezwa kwa kifupi kama:

($KN_1$) + (Kanusho) (Kiungio Nomino ni) + $KN_2$. Mabano yanaeleza kuwa katika mazingira fulani vipashio vya ndani vinaweza kudondoshwa.

## 3.2 Kiungio cha kiambishi nafsi/ngeli:

Tungo Nomino hujipambanua kwa kuwepo na kiungio kiambishi nafsi/ngeli kama: tu, m, (wa), ki, vi, li, n.k. Viungio Nomino hivi tulivyovitaja hufanya kazi ya kiarifu katika tungo.

(xiii) Mimi ni mpishi ("ni nafsi ya kwanza umoja)

(xiv) Wewe u mwalimu

(xv) Hamisi yu mwalimu

(xvi) Sisi tu walimu

(xvii) Ninyi m wapishi

(xviii) Kikombe ki mezani

(xix) Jembe li shambani

Katika tungo hizo saba, zote zinakubalika kiupatanisho wa kisarufi. Ingawa katika matumizi, baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili[4] hawakubali usahihi wa baadhi ya sentensi hizo kwa msingi kwamba hazitumiki sana siku hizi. Hapa itabidi tudokeze kwamba suala la "usahihi na

kukubalika" (grammaticality and acceptability) katika tungo hutegemea mambo mengi kwa pamoja. Mambo kama vile: uzoefu wa wazungumzaji; viwango vya elimu na ujuzi wa lugha; mahali watu hao waishipo; wakati n.k. haya hayana budi kutiliwa maanani na kuwa vigezo vya kutumika katika kukubali usahihi wa tungo hizo.

Kuhusu matumizi ya kiambishi nafsi (wa) wingi ni kwamba hakifuati upatanisho wa kisarufi na hata kimatumizi haikubaliki. Tukichukua mifano hii miwili:

(xx) Sisi <u>tu</u> walevi

(xxi) Sisi <u>wa</u> walevi

utaona kuwa sentensi ya (xx) inakubalika, lakini tungo ya (xxi) haikubaliki kimatumizi ingawa inafuata kanuni za upatanisho wa kisarufi. Tungo zenye kiungio cha kiambishi nafsi/ngeli zaweza kuwakilishwa kwa muundo ufuatao:

(KN) + (Kanusho) + (Kiambishi nafsi/ngeli) + $KN_2$

## 3.3 Kiungio cha Kiambishi nafsi/ngeli +mo, po, ko


Sifa nyingine ya tungo Nomino ni ile ya kuwa na kiungio nomino ambacho ni kiambishi nafsi/ngeli cha $KN_1$ pamoja na viangama vya mahali (-mo, -po, -ko). Kwa mujibu wa maelezo haya, tunaweza kuwa na viungio nomino kama: yumo, yupo, wamo, wapo, nipo, lipo, n.k.
Mifano ya tungo za namna hii ni kama ifuatavyo:

(xxii) Mtoto <u>yumo</u> ndani

(xxiii) Wageni <u>wapo</u> hapa

(xxiv) Juma <u>yuko</u> uwanjani

Katika lugha ya Kiswahili, kila kiangama cha mahali (mo, po, ko) katika tungo hutoa kivuli chake cha maana kama kielelezo hapa chini kinavyoonyesha.



Kiangama cha mahali -mo/mu hutoa dhana inayoeleza kuwa kitu kiko ndani. -po/pa, hueleza dhana ya kitu ambacho kiko karibu na mzungumzaji, ambapo -ko/ku, husaidia kueleza kuwa kitu kiko mbali kutoka kwa mzungumzaji. Kwa kifupi, tunaweza kuonyesha muundo wa tungo hizi kama ifuatavyo:

($KN_1$) + (Kanusho) + Kiambishi nafsi/ngeli + mo, po, ko + $KN_2$
Hata hivyo, katika tungo za aina hii, $KN_2$ chaweza kudondoshwa ikiwa taarifa ya $KN_1$ inafahamika na mzungumzaji..

(a) Juma yupo nyumbani?

(b) Msanjila yuko ofisini

(xxv a) (Ndiyo) yupo

(xxv b) Nipo (mimi mwenyewe)

Katika mtazamo wa kiisimu, "yupo" na "nipo" ni sentensi kamili kwa msingi kwamba tungo zote lazima ziwe na kiarifu, na yupo, nipo ni viarifu. Si nia ya makala haya kuingia kwa undani katika kipengele hiki, hata hivyo nitadokeza vipashio ambavyo vinaweza kukaa katika nafasi ya $KN_2$. Katika aina hii ya tungo nafasi ya $KN_2$ yaweza kukaliwa na:

(i) Nomino ambayo huongezewa ni mwishoni[5].

(xxvi) Watoto wako shambani

(xxvii) Mama yumo jikoni

(xxviii) Mwalimu yupo shuleni

(ii) Kihusishi (preposition) + Nomino

(xxix) Mpira uko chini ya meza

(xxx) Mama yuko katika likizo

(xxxi) Mchele haumo ndani ya kabati

(iii) Kiwakilishi cha mahali

(xxxii) Kiti chako kipo hapa

(xxxiii) Mtoto yupo pale

(xxxiv) Mgeni yuko mbali

(iv) Jina la mahali

(xxxv) Rais yuko Dodoma

(xxxvi) Unyonyaji haupo Tanzania

(v) Wakati mwingine kama tulivyokwisha sema, $KN_2$ chaweza kudondoshwa ($KN_2$ = Ø)

(xxxvi) (Mwalimu) yupo

(xxxvii) (vitu) vipo

## 3.4 Kiungio Nomino cha Kiambishi nafsi/ngeli + na

Katika kuzipambanua tungo nomino, sifa nyingine ni hii ya kuwa na kiungio ambacho ni kiambishi nafsi/ngeli + na

(xxxviii) Hamisi ana gari

(xxxix) Wanafunzi wa shule wana shamba kubwa

(xL) Wewe una nyumba ya kupangisha

(xLi) Mimi nina magari mawili

Viungio Nomino hivi: nina, ana, wana, n.k. vyote vinadokeza dhana ya umilikaji wa kitu.

## 3.5 Kiungio Nomino cha Ndi-/Si-

Kiungio Nomino cha Ndi-/Si-, hudokeza dhana ya msisitizo au mkazo katika tungo za Kiswahili. Katika tungo za namna hii Ndi-/Si- huenda pamoja na Viambishi rejeshi na viangama vingine.

(xLii) Mtoto mvivu ndiye huyu

(xLiii) Huyu siye mwizi

(xLiv) Kijiko kidogo ndicho hiki

(xLv) Kule ndiko mjini

Muundo huu huonyeshwa kama::

$(KN_1)$ + ndi-/si- mofimu rejeshi na viangama + $KN_2$

Kwa mujibu wa (Closs-Kondo -Mbaye), ndi/si na ndiyo/siyo huwa na dhima nyingine licha ya ile ya msisitizo. Kwanza wanadai kuwa ndiyo/siyo hutoa maana ya kukubaliana au kutokubaliana. Pili, ndio/sio hudokeza dhana ya kutoa ufafanuzi (definition).

(xLvi) Simoni ndiyo (ni) mwanafunzi (kukubali)

(xLvii) Simoni siyo (ni) mwanafunzi (kutokubaliana)

(xLviii) Chiriku ndio ndege (ufafanuzi)

Si nia ya makala haya kujadili maana na tofauti kati ya ndiyo/ndio, ila makusudi yalikuwa ni kujaribu kuonyesha kuwa ndi-/si- ni viungio nomino ambavyo hutoa maana iliyo tofauti na ile ya viungio nomino vilivyokwisha jadiliwa. Katika mazingira mengine ndiyo/ndio na siyo/sio huweza kuwa na maana zaidi ya hizi tulizozionyesha.

## 3.6 Kiungio Nomino cha "-ngali"

-ngali, ni kiungio nomino kimojawapo kinachounga $KN_1$ na $KN_2$ na kinaonyesha hali ya kitu (qualification) na pia kinaonyesha mahali.

(xLix) Juma yungali mwanafunzi

(Lx) Sisi tungali shambani

(Lxi) Mtoto wetu angali mgonjwa

(Lxii) Mama angali nyumbani

Sentensi hizi zaweza kuonyeshwa kwa kifupi kama:

($KN_1$) + (Kanusho) + kiambishi nafsi/ngeli + ngali + $KN_2$.

## 3.7 Kiungio cha -kuwa

-KUWA, ni kitambulisho kimojawapo cha tungo nomino. Hufanya kazi ya kuarifu juu ya $KN_2$

(Lxiii) Bakari atakuwa mwalimu

(Lxiv) Baba alikuwa mkulima

Sentensi ya (Lxiii) hapo juu inaarifu kwamba Bakari atakuwa mwalimu hapo baadaye (wakati ujao). Sentensi ya (Lxiv) inaarifu juu ya kazi aliyokuwa anafanya Baba kwa siku za nyuma (wakati uliopita).

Tumekwisha sema kwamba kitenzi -KUWA na "vitenzi -ungio" vyote ni kopula. Hoja hii inaibua swali moja la msingi juu ya matumizi ya pamoja ya -KUWA na ni. Hebu tuangalie sentensi hii.

(Lxv) Baba alikuwa ni mkulima.

Sentensi hii imetumia vipashio vyote viwili -kuwa na ni. Maswali ambayo wanaisimu wamekuwa wakijiuliza ni haya:

(a) je, -"kuwa" na "ni" katika sentensi (Lxv) hapo juu zote ni kopula? (Wesana-Chomi; 1978:38)

(b) nini kazi ya "kuwa" na "ni" katika sentensi hiyo?

Ingawa si nia ya makala haya kujadili kwa undani tofauti hizi, lakini itatubidi tuziangalie upya sentensi za namna hiyo kwa ufupi. Sentensi ya (Lxv) inaweza kuandikwa kwa namna mbili zaidi:

(Lxvi) Baba alikuwa mkulima

(Lxvii) Baba ni mkulima

Sentensi zote mbili (Lxvi na Lxvii) zinaarifu juu ya kazi ya baba (mkulima). Tukirudi nyuma kuichunguza sentensi yetu ya (Lxv), tunaona kwamba matumizi ya "ni" siyo ya lazima sana kuwepo.

Baba alikuwa (ni) mkulima

Mtu hahitaji msaada wa kopula ni ndipo aelewe maana ya sentensi hiyo. Vile vile matumizi ya -kuwa siyo ya lazima kuwepo ikiwa maana inayotakiwa ni ya wakati wa sasa.

yaani, Baba (alikuwa) ni mkulima.

Kutokana na ufafanuzi huu, tunaweza kusema kwamba katika sentensi ya (LXV) -kuwa ni kopula kwa sababu ni kiungo cha lazima kuwepo katika sentensi hiyo ili kutoa maana iliyokusudiwa. Kama ni lazima "ni" kutumika pamoja na -"kuwa", basi "ni" siyo kopula bali ni kipashio kinachofanya kazi ya msisitizo juu ya $KN_2$ "Baba alikuwa ni mkulima", hapa ina maana kwamba Baba hakuwa na kazi nyingine yeyote ila ya ukulima tu.

## 4.1 Muundo wa Tungo

Kama tulivyokwisha sema, tungo nomino zina muundo rahisi na hujengwa na vipashio vifuatavyo:

$(KN_1)$ + (Kanusho) (Kopula) + $KN_2$

Kwa upande mwingine, tungo vitenzi zina muundo ambao huweza kuwa sahili au changamano. Muundo wenyewe huonyeshwa kama:

K + A + Sh (ch)

K = Kiima, A = Kiarifu

Sh = Shamirisho, Ch = Chagizo

(Lxviii) Mpishi/anapika/chai (K + A + Sh)

(Lxix) Juma/amefika/shuleni jana (K + A + Ch)

(Lxx) A/mekuja/mara mbili (K + A + Ch)

## 4.2 Nyakati katika Tungo

Tungo nomino zinatumia nyakati chache na aghalabu huwa ni tatu ambazo ni: wakati uliopo; uliopita na ujao.

(Lxxi) Hamisi ni mwalimu (wakati uliopo)

(Lxxii) Hamisi alikuwa mwalimu (wakati uliopita)

(Lxxiii) Hamisi atakuwa mwalimu (wakati ujao)

Kwa upande wa tungo vitenzi ni kwamba hakuna mpaka wa matumizi ya nyakati, nyakati zote huweza kutumika.

## 4.3 Upatanisho wa Kisarufi katika Tungo

Kama tulivyokwisha sema awali, tungo nomino zina mpaka wa matumizi ya kisarufi. Kwa mfano, kiambishi nafsi cha tatu wingi "wa", hakisadifu upatanisho wa kisarufi kikitumiwa kama kiungo nomino cha tungo.

Mfano wa (xxi) uliotolewa katika hatua ya 3.2 unadhihirisha hoja hii. Viambishi nafsi vingine hukidhi upatanisho wa kisarufi ingawa kuna baadhi ya wazungumzaji wa Kiswahili ambao wanaona mashaka juu ya usahihi wa matumizi ya tungo hizo (Closs-Kondo-Mbaye 1967:7). Kwa mifano zaidi tazama nyuma katika hatua ya 3.2, mifano ya xiii-xix inafaa.

Katika tungo vitenzi hakuna mipaka ya upatanisho wa kisarufi. Upatanisho wa kisarufi na viambishi nafsi/ngeli husadifu vizuri na bila mashaka yoyote kwa wazungumzaji wa Kiswahili. Ifuatayo ni mifano michache inayoonyesha upatanisho wa kisarufi katika vipashio vinavyofuatana.

(Lxxiv) Mtoto mzuri amefika leo

(Lxxv) Watoto wazuri wamefika leo

(Lxxvi) Yule mpishi hakupika chakula

(Lxxvii) Wale wapishi hawakupika chakula

## 4.4 Upanuzi wa Tungo

Katika tungo nomino za Kiswahili, $KN_1$ na $KN_2$ ndizo huweza kupanuliwa. Upanuzi huu hufanywa kwa kutumia dhana ya urejeshi ambayo hujitambulisha kwa umbo la msingi la "amba-" na kufuatiwa na mofimu za urejeshi za:-ye; -o; -lo; n.k.

(Lxxvii) Juma ambaye anakaa Tabora/ni mwizi sana

(Lxxix) Watoto waliotoka Dodoma/ni/wanafunzi wasomao darasa la saba

(Lxxx) Timu ya mpira ambayo iko Tanzania/itakuwa/na mchezo mkali ambao haujawahi kutokea.

Pia tungo nomino huweza kupanuliwa kwa kutumia a- unganifu

(Lxxxi) Hamisi, Juma na Ali/ni/wanafunzi wa darasa la kumi

(Lxxxii) Mwalimu mkuu wa shule ya Iyoma/ni/ mcheshi na (ni) mpole.

Katika tungo vitenzi licha ya upanuzi wa kufanywa na $KN_1$ na $KN_2$ pia huweza kufanywa kwa kunyambulisha kitenzi kamili.

(Lxxxiii) Juma anachezea mpira

(Lxxxiv) Watoto wanamlimia babu yao shamba lake

Katika sentensi za hapo juu, vitenzi "cheza" na "lima" vimeweza kunyambulishwa na kuwa "chezea" na "limia". Kwa upande wa tungo nomino, "kiungio nomino" ambacho ndicho kitenzi cha sentensi huwa hakiwezi kunyambulishwa.

## 4.5 Dhana ya Kitendo katika Kitenzi

Vitenzi vinavyotumika katika tungo nomino havionyeshi kitendo kinachofanyika, bali huonyesha kuwepo kwa kitu fulani, hali ya kitu, sifa yake, hali ya udhihirisho, na pia huonyesha uwiano kati ya vitu.

(Lxxxv) Baba amekuwa anaumwa kwa siku nyingi (hali)

(Lxxxvi) Sofia awa mtoto mwema (sifa)

(Lxxxvii) Ali ni mwalimu wa Chuo Kikuu (udhihirisho)

Kwa upande wa tungo vitenzi ni kwamba vitenzi vyake huonyesha kitendo kinachofanyika. Dhana ya mtenda na mtendwa hujidhihirisha kwa wazi. Hata hivyo katika tungo vitenzi vipo vitenzi ambavyo havionyeshi kitendo bali huonyesha sifa kama za vitenzi -KUWA na vitenzi -UNGIO.

(Lxxxviii) Juma amelala fofofo

(Lxxxix) Pipa limejaa maji

(Xc) Mzee amefurahi sana

Vitenzi kamili, amelala, limejaa, amefurahi ni baadhi tu ya vitenzi kamili visivyoonyesha kitendo lakini vyenyewe siyo vitenzi vya tungo nomino. Hebu tuangalie mifano hii:

(xci) Baba ni mgonjwa

(xcii) Baba amekuwa mgonjwa

(xciii) Baba amelala mgonjwa

Katika sentensi ya (xci) na (xcii) kitenzi -ungio ni na kitenzi KUWA vyote vinaarifu hali ya baba ilivyo; Baba

siyo mzima, bali ni mgonjwa. Sentensi ya (xciii) kitenzi amelala kinaeleza habari zaidi ya hali ya baba; baba siyo mgonjwa tu bali amelala, hatembei wala hasimami. Maana hizi za ziada hazipatikani kwenye sentensi za (xci) na (xcii) za tungo nomino, isipokuwa kwenye tungo zenye vitenzi kamili tu. Kisarufi, vitenzi-ungio, kitenzi KUWA na vitenzi kamili vyote, hufanya kazi moja ya kiarifu (predicate) katika tungo.

## 4.6 Uwezo wa Vitenzi kupokea Viambishi

(xciv) Mtoto alikuwa mgonjwa (a-li-)

(xcv) Juma amekuwaje usoni (a-me-je)

(xcvi) Baba hakuwa shambani (ha-)

-je, ni kiambishi tamati kiangama kimojawapo.

Tungo nomino pia hutumia viambishi tamati - maana tu vinavyoeleza hali yakinishi na kanushi. Vile vile, tungo nomino hutumia viambishi rejeshi na viambishi vinavyoonyesha nia - kama vile ya kuamuru au kuuliza.

(xcvii) Mwalimu hawi mvivu (kanushi)

(xcviii) Mtoto awa mchangamfu (yakinishi)

(xcix) Juma amekuwaje kichwani (kuuliza)

(c) Aliyekuwepo ni mzee wa Tanga (rejeshi)

Kwa upande wa tungo vitenzi, matumizi ya viambishi vya aina mbalimbali hutumika kwa wingi sana kutegemeana na aina ya kitenzi na maana ya tungo ikusudiwayo. Mifano ya namna hii ni mingi sana katika sentensi za Kiswahili.

## 5.0 Hitimisho

Mpaka sasa tunaweza kusema kwamba tungo nomino hutofautiana na tungo vitenzi kutokana na matumizi ya kitenzi KUWA na vitenzi -ungio. Tunaviita vitenzi -ungio kwa msingi kwamba vikikaa peke yake siyo vitenzi kamili bali ni viungio vya tungo, na si viungio tu, bali ni viungio vinavyofanya kazi ya kuarifu juu ya $KN_1$ na $KN_2$. Kitenzi KUWA na vitenzi -ungio, vyote kwa pamoja hufanya vitenzi vya tungo nomino, vitenzi ambavyo hutofautiana na vitenzi kamili vya kwenye tungo vitenzi.

MAREJEO

1. Kopula ni kijineno cha kitenzi KUWA kinachotumiwa kuunganisha KIARIFU (Predicate) na KIIMA katika tungo nomino.

2. "Kitenzi-ungio" ni kopula yeyote isiyochukua umbo la KUWA katika tungo nomino.

3. "Kitenzi kamili", hapa na kusudia ni kile kitenzi kinachoonyesha kitendo na kina sifa zote za kitenzi kama vile: kionyesha mtendaji wa tendo; idadi ya watendaji; wakati hauna budi ujulikane pamoja na hali ya kitendo; tendo lijulikane wazi, taarifa hakina budi kionyeshe kama ni maelezo, swali, amri au hata mshangao.

4. Closs-Kondo-Mbaye (1967) "Some copula patterns in Standard Swahili" SWAHILI journal, Vol. 37/1 uk. 7.

5. Nomino zinazoweza kuongezewa -ni mwishoni ni Nomino zote isipokuwa za "proper nouns".